TANGAZO LA SERIKALI NA. 840 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8 (1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NJIA PANDA YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga eneo la Njia Panda ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Maswa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA69 yenye majira - nukta 568407MS, 9647661KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa uelekeo KZ68$^{0}$06'05"MS kwa umbali wa kilomita 2.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA84 yenye majira – nukta 571020MS, 9648711KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS110$^{0}$10'16"MS kwa umbali wa kilomita 1.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VM 709 yenye majira – nukta 572031MS, 9648340KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS98$^{0}$47'00"MS kwa umbali wa kilomita 1.04 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VM708 yenye majira – nukta 573073MS, 9648179KZ; baada ya hapo mpaka

*Tangazo la Serikali Na. 840 (Linaendelea)*

unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KS85$^0$03'52"MS kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VM 728 yenye majira – nukta 574370MS, 9648291KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS217$^0$31'27"MG kwa umbali wa kilomita 6.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA130 yenye majira – nukta 570663MS, 9643465KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Magharibi katika uelekeo wa KS282$^0$53'12"MG kwa umbali wa kilomita 5.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA 68 yenye majira – nukta 565527MS, 9644640KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ43$^0$38'25"MS kwa umbali wa kilomita 3.02 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*